# Waongoza Njia wa Mfumo wa Afya
# Kukusaidia na matunzo yako ya afya

phn MURRAY
An Australian Government Initiative

## Je, Waongoza Njia wa Mfumo wa Afya ni nini?

Mwongoza Njia ni mtu anayekusaidia kupata huduma za kutunza afya unazohitaji. Anakusaidia kushinda vizuizi vya kupata huduma ya afya, inayorahisisha kwako kupata huduma unayohitaji kwa jinsi inavyoheshima utamaduni wako.

Mwongoza njia kwa kawaida wametoka asili za uhamiaji au ukimbizi, na wengine wanasema lugha nyingine. Huduma ni bure na inafadhiliwa na Murray PHN.

## Je, inafanyaje kazi?

**Unganishwa na huduma:** Unaweza kuomba usaidizi wewe mwenyewe au mtoa wako wa huduma ya afya, daktari, shirika la eneo au mtu unayemjua anaweza kukurejelea.

**Kutana na Mwongoza Njia:** Mwongoza Njia anaweza kukutana nawe katika mahali ambapo ni rahisi kwako. Atakuuliza maswali ili kuelewa mahitaji yako ya afya.

**Pata usaidizi:** Mwongoza Njia atajaribu kukusaidia kupata huduma za afya, kukusaidia kujaza fomu, kupanga miadi ya kimatibabu na kukupa taarifa ya afya.

*Kumbuka: Waongoza Njia sio madaktari. Hawatoi ushauri au tibu ya kimatibabu. Wanakusaidia kupata huduma na usaidizi sahihi lakini hawatibu hali za afya.*

## Je, Mwongoza Njia anaweza kutoa usaidizi gani?

Mwongoza Njia anaweza:

- kuunganisha wewe na huduma za afya zinazoridhi mahitaji yako
- kukusaidia kupanga na kuhudhuria miadi ya kimatibabu
- kusaidia kujaza fomu
- kutoa taarifa iliyotafsiriwa ya afya
- kuunganisha wewe na huduma nyingine
- kukusaidia na mahitaji ya kila siku yanayoathiri afya yako na ufikiaji kwa huduma

## Nani anaweza kuwasiliana na Mwongoza Njia?

Unaweza kuwasiliana na Mwongoza Njia ikiwa wewe umetoka jamii ya tamaduni nyingi - kama mkimbizi, mtafutaji hifadhi, au mhamiaji mwingine - na unakabiliana na changamoto yoyote yafuatayo:

- inakuwa ngumu kupata huduma za afya kutokana na vizuizi vya kilugha, kitamaduni, au vizuizi vingine
- mahitaji magumu ya afya au yanayoendelea
- lugha yako ya Kiingereza ni kidogo
- wewe ni mgeni mpya nchini Australia
- unaishi eneo la vijijini



## Huduma za Mwongoza Njia wa Mfumo wa Afya katika eneo lako

| | |
|---|---|
| **Bendigo** | **Huduma za Afya ya Jamii za Bendigo**<br>171 Hargreaves Street, Bendigo VIC<br>Simu: 03 5406 1200<br>Barua pepe: bchs@bchs.com.au |
| **Shepparton** | **Miunganisho wa Huduma ya Msingi (Primary Care Connect)**<br>399 Wyndham Street, Shepparton VIC<br>Simu 03 5823 3200<br>Barua Pepe: intake@primarycareconnect.com.au |
| **Robinvale** | **Huduma za Afya ya Wilaya ya Robinvale**<br>128 Latje Road, Robinvale VIC<br>Simu: 03 5051 8160<br>Barua pepe: primarycare@rdhs.com.au |

Kwa maelezo zaidi, tembelea: murrayphn.org.au/community/multicultural-health/

## Maelezo muhimu

- Ni chaguo lako tu kama unataka kumwona Mwongoza njia.
- Hakuna gharama kumwona mwongoza njia.

Ikiwa una maswali yoyote, tuma barua pepe kwa Murray PHN kwa: multicultural@murrayphn.org.au

## Je, unahitaji mkalimani?

Tafadhali mwambia mtoa huduma ikiwa unahitaji mkalimani.

**Piga simu kwa 131 450** (Huduma ya Tafsiri na Ukalimani) na uliza kupata mkalimani.

